

## KUFUNGULIWA KWA MIHURI SABA (SIYO SITA) KUNATIMIZA UFUNUO 10

### Ufunuo 8:1

*“Hata alipoifungua muhuri ya saba, kukawa na kimya Mbinguni kama muda wa nusu saa”.*

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema:

Tangu kufunguliwa kwa mihuri hii saba, ya wale malaika saba nyuma ya mlima ng’ambo kule, hiki kimekuwa kitabu kipya. Ni yale mambo ambayo yalikuwa yamefichwa na sasa yanafunuliwa kama Mungu alivyoahidi katika ufunuo 10 kwamba atayafanya.

Na sisi ni watu tuliotunukiwa ambao Mungu amewachagua duniani, kwamba tuweze kuyaona na kuyaelewa mambo haya; ambayo siyo uzushi, akili za kimwili za mtu anayejaribu kuunda vitu. Ni neno la Mungu likidhihirishwa, likithibitishwa kwamba ni kweli. Likithibitishwa, siyo na sayansi ila na Mungu kuwa ni kweli.

Mungu habitaji mtu yeyote atafsiri Neno lake. Yeye ni mtafsiri wake mwenyewe. Ananena kuwa litafanyika, na linafanyika. Analithibitisha hilo; na hiyo inalitafsiri hilo. [1]

Halafu nyuma kule mwanzoni mwa mihuri saba, wakati wale Malaika saba waliposhuka chini katika umbile la piramid, walisimama pale, na kuniambia nirudi hapa (maskanini) na nizungumze juu ya hiyo mihuri saba. Naye atakuwa na mimi. Alinionyesha mimi ilikuwa ni kitu gani, mambo yaliyo potezwa. Siku zote niliwaza yalifungwa nyuma ya kitabu na kwamba ingekuwa kitu fulani ambacho hakikuandikwa katika kitabu; lakini alinionyesha na kunijulisha kuwa hawezi kufanya hivyo. Siyo kitu ambacho kiliandikwa katika kitabu .....Ni kitu fulani ambacho kilifichwa katika kitabu: “Kwa kuwa mtu yeyote akiondoa Neno moja kutoka humo au akiongeza Neno moja katika hilo..... “(ufunuo 22:18-19).

Kwa hiyo ilikuwa ni siri ambayo ilikuwa katika kitabu wakati wa nyakati hizi saba za kanisa. Kila mmoja ilileta siri, yote kuhusu ubatizo wa maji, na mambo haya mengine ambayo yamewatatanisha kwa muda mrefu sana. [2]

Sasa, angalia wakati wa kufunuliwa kwa mihuri saba, ufunuo 10, Neno, lote litazaliwa na kudhihirishwa tena na kuthibitishwa na Roho wa Mungu katika nguvu yote, kama tu ilivyokuwa hapo alipokuwa hapa duniani. Amina. Waebrania 13:8 ilisema Yesu Kristo yule jana, leo, na hata milele. Katika Luka 17:30 Yesu alisema, “katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa siku za sodoma wakati mwana wa Adamu atakapojifunua Mwenyewe tena. Itakuwa ni jambo lile lile” [3]

Angalia lile ono la Tuksoni miaka mitatu iliyopita. Nami nililingia ndani kuangalia katika kitabu changu kidogo; lilikuwa pale. Na asubuhi iliyofuata saa kumi wakati Malaika wa Bwana aliposhuka chini pale chumbani na Akasema, “Nenda Arizona. Utakuwa Kaskazini Mashariki mwa Arizona na hapo watakuja Malaika saba wakiwa kundi moja ambalo litatikisa nchi yote inayokuzunguka wewe”. Na akasema, “utaambiwa kutoka hapo”.

Ni wangapi hapa wanakumbuka hayo, mbali kabla hayajatokea? Kuna watu waliokaa hapa kati yenu usiku wa leo katika jengo hili waliokuwa wamesimama pale wakati hayo yalitokea, na akasema ile mihuri saba ya Siri zilizo fichika za Biblia yote zitafunguliwa na kutimiza ufunuo 10, huo ni ujumbe wa Malaika wa saba, ambapo haya mambo yatakuja kutimia. Leo haya maandiko yanatimia mbele ya macho yetu. Leo hii haya maandiko yanatimia. [4]

Biblia ilisema katika malaki 4, kile kitakacho tokea leo, Ufunuo 10, jinsi ambavyo ile mihuri saba itakavyo funguliwa na kufunua siri hizi zote ambazo zilikuwa zimefichwa kupitia hawa watengenezaji. Alisema vile itakavyofanyika. Iko katika Biblia, HII ASEMA BWANA. Mungu amemaliza, kikamilifu kulitambulisha hilo na kulithibitisha kwamba ni kweli kwa Ishara, na maajabu katika mbingu na mawinguni, na kila kitu kingine kwa miaka –thelethini na tatu. Unafikiri watasikiliza hilo? Hapana, wamekufa. Wameweka mikono yao katika kitu fulani ambacho kimeua kitu chote. Hapana, haitaweza tena kamwe.

Wakati wa jioni, aliahidi atafunua – kuweka wazi hii mihuri saba na kuonyesha yale Makanisa yalicho kikosa pale nyuma. Ufunuo 10, na Malaki 4, Luka 17:30, Alisema angelitenda hilo, kwa hiyo tusichanganye hilo. Hebu tuliweke kwa usahihi kama hivyo. [5].

Angalia siku ile hasa yule mjumbe, siyo atakapo anza kwenye... lakini atakapoanza kutangaza ujumbe wake. Unaona? Mvuto wa kwanza, uponyaji; Mvuto wa pili, kutoa unabii; Mvuto wa tatu, kufunguliwa kwa Neno; zile siri zilifunuliwa. Hakuna kiwango cha juu cha kufunua Neno zaidi ya Manabii. (Amosi 3:6-7) . lakini njia pekee ambayo nabii anaweza kuthibitishwa ni kwa Neno. Na kumbuka mvuto wa tatu ni kufunuliwa kwa ile mihuri saba kufunua kweli zilizofichwa ambazo zilikuwa zimefungwa katika Neno. Unalionga [6]

Kumetokea nini kule mlima wa (sun set) macheo ya jua? Mungu akithibitisha Neno lake. Hiyo ndiyo sababu ya makelele hayo. Angalia ni Mungu akitimiza ahadi zake za Neno tena, la Ufunuo 10:1-7. Na katika siku za ujumbe wa malaika wa saba, siri za Mungu zitakuwa zimemalizika “(zimekwisha)”. Zile siri zilizofichika za Ufunuo 10:1-7, ujumbe wa mwisho kwa kanisa la wakati wa mwisho. Inatimiza kabisa, katika wakati huo Luka Mt:17:30, “siku ambayo Mwana wa Adamu atakuwa anafunuliwa”.

“Na hapo watainuka manabii wa uongo na makristo wa uongo wakionyesha ishara kuu na maajabu kiasi chakuweza kumdanganya mteule kama ingewezekana”. (Mathayo 24:24) watu bado wako kwenye mashaka. Na kama kawaida, kanisa limeshikwa na mshangao. [7]

Na hapo sasa hiyo inapokuja, Akafungua mihuri saba na akafunua nuru ya wakati wa jioni, akichukuwa siri zote ambazo zilikuwa zimefichwa katika nyakati hizi za kanisa na sasa anazifunua kama alivyo ahidi katika ufunuo 10:1-7.

Tuko hapa leo, tukiwa tumeketi katikati ya Neno, na Neno lilikuwa linafunuliwa kwetu na Yesu Kristo kwa hiyo hili ni Neno la Mungu. [8].

Kitabu cha Ufunuo ni kitabu cha mwisho cha Biblia. Kimefungwa (kutiwa muhuri) kwa wasioamini. Pale ndani katika Ufunuo sura ya 22 mstari wa 18-19.

“Mtu yoyote akiyaongeza, Mungu atamuongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki, Mungu atamuondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima”. Tunatambua kwamba kwa ujumla kilitolewa kwa ajili ya waaminio. Na kinafungua kitabu cha ufunuo na kumfunua yule mwandishi wa kitabu chote kuwa ni (Ataonekana kama Alfa na Omega, kutoka mwanzo mpaka ufunuo. Yesu Kristo aliye yule yule tu na limenyoka kote) na anafunua kikamilifu siri ya Yeye mwenyewe na mpango wake kwa nyakati za kanisa ambazo zingekuja baadaye, na zilifungwa pale na mihuri saba.

Sasa, kile kitabu kiliandikwa, lakini ukumbuke kilikuwa kimefungwa na mihuri saba (Ufunuo 5:1-5).

Na hii mihuri saba ilikuwa isifunguliwe, Ufunuo 10, mpaka wakati wa baragumu ya mwisho ya malaika yule wa duniani hapa duniani Ufunuo 10:7. “Na katika siku za sauti ya ujumbe wa malaika wa mwisho malaika wa saba, siri ya Mungu itakuwa imemalizika katika wakati huo”. Na huo ni wakati wa sasa ambao tunaishi.

Sisi sote tunajua tunaishi katika wakati wa laodikia. Kamwe hakutakuwa na wakati mwingine zaidi ya huu haiwezekani. Kwa hiyo tunaishi katika wakati wa laodikia na hii mihuri saba ambayo imekishikilia kitabu ni Siri kwa watu, itafunguliwa katika siku ile. Hivyo ndivyo alivyo ahidi. Sasa haitakuwa kitu fulani nje ya Neno kwa sababu huwezi kuongeza kwenye Neno au kupunguza katika Neno. Inabidi siku zote ibakie kuwa

Neno. Lakini ule Ufunuo unafunua ukweli wake, ni nini? Kuifanya ikubaliane na maandiko mengineyo yote. Na halafu Mungu analithibitisha kuwa hilo ni kweli [9].

Sasa huyu mjumbe wa malaika 4 na ufunuo 10:7 ataenda kufanya mambo mawili,

Moja: kulingana na malaika 4, ataigeuza mioyo ya watoto kuwaelekea mababa.

Mbili: Atafunua siri ya ngurumo saba katika ufunuo 10:3-4 ambazo ni mafunuo yaliyo katika mihuri saba. Itakuwa ni hizi “kweli za siri” zikifunuliwa kiungu ambazo zinageuza mioyo ya watoto kuwageukia Baba zao wa Kipentecoste hiyo hasa ndivyo ilivyo. [10].

Kitabu hiki cha mihuri –saba, kinafunuliwa wakati wa zile ngurumo saba za Ufunuo10. Kama unaandika hilo..... hebu tufungue Ufunuo 10 kwa mara moja, iliupate ufahamu kabla hatujalifikia hilo. Hili ni wakati wa mwisho, sikiliza- “....Nikamuona Malaika mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni akiwa amevikwa wingu na upinde wa mvua-----juu ya kichwa chake”.

Kama ukiangalia huyo ni Kristo, kwa sababu Yeye katika Agano la kale aliitwa Malaika wa Agano na Yeye anakuja moja kwa moja kwa wayahudi sasa, kwa maana wakati wa kanisa umeisha. Unaona? Vema---- na uso wake-- ulikuwa kama jua na miguu yake kama nguzo za moto”.

Unamkumbuka yule Malaika katika ufunuo 1? Jambo lile lile. Malaika ni mjumbe na Yeye ni mjumbe kwa Israeli. Unaona? Kanisa tayari limenyakuliwa sasa, unaona? au linataka kunyakuliwa. Anakuja kwa kanisa lake.

Sasa, unaona, siri ya kitabu hiki cha mihuri saba kitafunuliwa wakati wa sauti(baragumu) ya Malaika wa kanisa la saba. Unaona? Malaika wa saba anaanza kupiga baragumu, na unaona pale kuna ujumbe unaona? Malaika wa saba anaanza kupiga baragumu, na pale upo ule ujumbe ukiwa umeandikwa na tunazo kanda na vitabu pale na tunavyo katika kanda na kitabu.

Sasa, pale mwanzoni mwa ujumbe, ile siri ya Mungu inapaswa iwe imemalizika katika wakati huo. Sasa, tunaona kwamba, kile kitabu cha siri za Mungu hakifunuliwi mpaka ule ujumbe wa Malaika wa saba umeanza kutolewa.

Sasa, hizi pointi zitakuwa muhimu sana katika mihuri; nina uhakika, kwa sababu lazima kila kifungu vikubaliane pamoja. Sasa, vimeandikwa kisiri, kwa sababu hakuna mtu popote anayejua hilo: Mungu pekee, Yesu Kristo.

Lakini sasa ni kitabu, kitabu cha siri. Ni kitabu cha ukombozi. Na sasa, tunajua hiki kitabu cha ukombozi hakitaeleweka vizuri; kitapapaswapapaswa katika nyakati sita za kanisa, lakini wakati wa mwisho, wakati Malaika wa

saba atakapoanza kutoa zile siri zake, atachukuwa vipengele vyote vilivyoachwa ambavyo watu walipapasapapasa, na ile siri inakuja kutoka kwa Mungu kama Neno la Mungu na inafunua ufunuo wote wa Mungu. Halafu Uungu, na kila kitu kingine vinawekwa vizuri. Siri zote. Uzao wa nyoka na chochote kile ambacho kinatakiwa kifunuliwe. [11].

Na sasa angalia kunakitu fulani sio sahihi mahali fulani katika makanisa. Na ninafikiri ni utaratibu wa kidhehebu ambao unayumbisha yumbisha akili za watu na kadhalika mpaka hawajui namna ya kufanya, hiyo ni kweli. Lakini tumeahidiwa kuwa itafunuliwa.

Na sasa, hii mihuri saba ambayo hiki kitabu kimefungwa nayo, na hii mihuri saba..... Na baada ya kumalizika kwa hii mihuri saba, tunaona katika ufunuo 10 kuna ngurumo saba za siri ambazo Yohana-aliagizwa aandike. Lakini hapo alikatazwa asiandike hizo. Na wakati wa hizo ngurumo, tunamuona Kristo, au Malaika akishuka chini akiwa na upinde wa mvua na akaweka mguu wake katika nchi na bahari na kuapa kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya.

Na halafu tunaona katika kule kufunuliwa kwa mihuri kwamba mwana kondoo ameondoka katika kiti chake cha rehema/upatanisho na amekuja sasa ili kudai haki zake, vile vyote alivyovikomboa kwa mauti yake. [12].

Sasa, anaenda kulionyesha kanisa kile alichokifanya. Unaona? Halafu tu anachukuwa..... Lakini kile kitabu kimefungwa (Ufuno 5:6-10). Hakuna hata mmoja ajuaye hata kidogo. Wanajua ni kitabu cha ukombozi juu pale, lakini inabidi kifunuliwe siku za mwisho kutokana na Ufunuo10, yule Malaika wa saba ataenda kupewa ujumbe wa hiyo, kwa sababu imesema kuwa katika sauti ya Malaika wa saba, atakapopiga baragumu yake, siri zote za Mungu zitakuwa zimekwisha kwa baragumu yake. Baada ya kufunuliwa, Malaika alishuka chini kutoka Mbinguni; ambaye alikuwa ni Kristo (sasa kumbuka, huyu Malaika naye yuko duniani, mjumbe). Kristo anashuka chini unamwona Yeye katika Ufunuo sura ya 10), Anaweka mguu mmoja juu ya nchi na mwingine baharini, na upinde wa mvua juu ya kichwa chake, macho kama mwali wa moto na miguu kama moto na kadhalika, anainua mikono yake juu na kuapa kwa Yeye aishiye milele na milele katika enzi yake kwamba hapatakuwa na wakati.

Na anapochukuwa hiki kiapo, ngurumo saba zinatoa sauti zao na yule mwandishi Ufunuo10:1-4, ambapo Yohana alipochukuliwa juu alipaswa kuandika alichokiona. Alianza kuandika chini. Akaambiwa “usiandike kwa sababu.... Usiandike hilo” Ni..... akasema “Yatie muhuri.” Nini? “Yatie muhuri usiseme kitu” unaona? Itafunuliwa, lakini haikuandikwa katika Neno. Na alipoanza kufunua mihuri, tunaona kwamba wote walikuwa wameshangazwa. [13].

Sasa, tunaona kwamba huu muhuri wa sita sasa ukiwa unafunuliwa (Ufunuo 6:12-17) ni kwa makusudi matatu. Sasa hapa tunaona yale makusudi: Jambo la kwanza ni kuwa Yule mwanamwali mpumbavu anapitia katika dhiki kuu kwa ajili ya kutakaswa. Inabidi atakaswe kwa ajili ya dhambi zake za kutokuamini na kwa kukataa ujumbe.

Hili linafanyika katika wakati wa dhiki kuu. Tunaona wanaonekana hapa katika ufunuo 7:13-17, katikati ya sura ya sita na sura ya saba, kwamba amekwisha kutakaswa na kupewa vazi lake.

Sasa, yeye sio Bibi Arusi, lakini ni kanisa, watu walio safi ambao hawakupata nafasi, na bado walikuwa watu waaminifu ndani ya mioyo yao, na Mungu anajua mioyo yao, na ndio hapa wametakaswa katika huo wakati.

Angalia wakati mwingine wa kutakaswa; Ni wakati Israeli wanapokusanyika, hiyo ni lile kusudi la pili Mungu anawatakaswa Israeli wakati wa dhiki kuu. Kati ya mamilioni watakaokusanyika pale, watakuwepo mia moja arobaini na nne elfu waliochaguliwa, ambao watatakaswa pia. Mungu anawatakaswa Israeli (Ufunuo7:1-8).

Angalia dunia yote itatakaswa. Kutakuwa na vitu kama mwezi, nyota, na vitu vyote vya asili vitatakaswa. Unaona ni nini? Dunia inajifanya upya yenyewe, kwa kutakaswa, ikiwekwa tayari kwa utawala wa miaka elfu moja. Miaka elfu moja inakuja. Na uone, kila kitu chenye uchafu ndani yake kitatakaswa wakati wa muhuri wa sita.

Sasa, sasa, umeona hili katika kufunguliwa kwa muhuri wa saba, nao pia upo katika makusudi matatu ya siri. Itakuwa wakati wa kuja kwa Kristo, kwa sababu Kristo alisema hakuna hata mmoja ajuaye Yeye atakapokuja (Matayo 24:36-42)

Je uliona hiki pale wayahudi walipomuuliza Yeye hilo? Unajua tunapolinganisha maandiko hapa na Matayo 24 na ile mihuri sita (Matayo 24:4-31). Ule muhuri wa saba uliachwa; kwa sababu (unaona?), Kristo alisema ni Mungu pekee mwenyewe ajuaye, hata Malaika hawajui. Sio ajabu ndio maana hata haikuandikwa. Unaona, walishangazwa, hakuna kilichoendelea hapo. Malaika hawajui hilo, hakuna ajuaye ni lini Yeye anakuja. Kutakuwa na sauti saba za ngurumo ambazo zitafunua ule ufunuo mkuu wakati huo.

Kwa hiyo ninaamini kwa sisi ambao.... Kama hatujui hilo na halitajulikana mpaka wakati huo. Lakini litafunuliwa katika siku hiyo. Katika saa ambayo linapaswa kufunuliwa. Kwa hiyo jambo tupaswalo sisi kufanya ni kuwa wanyenyekevu mbele za Mungu na kumtumikia Yeye, na kufanya yote tujuayo kuyafanya, na kuishi maisha mazuri ya Mkristo apaswavyo kuishi.

Hapa sasa tunaona muhuri wa sita umefunuliwa kwetu; tunaona hilo, na tunajua kwamba huu muhuri wa saba hauwezi kuvunjwa mbele ya watu

mpaka huo wakati ufike.

Sasa, kunasababu fulani ambayo ilimfanya Mungu aruhusu hizi sauti saba zingurume, kwa sababu lazima zije, kwa maana..... Tunaona kuwa Kristo, Mwanakondoo alichukuwa kitabu, mkononi mwake na akafungua ule muhuru wa saba. Lakini unaona? Ni siri iliyo fichwa. Hakuna hata mmoja ajuaye. Lakini inakubaliana na yale aliyosema: hakuna atakayejua saa ya kuja kwake; pia hawatajua juu ya siri ya ngurumo saba. Kwa hiyo unaona, vimeungana pamoja.

Tumeelewa kiasi hicho leo. Kwa sababu yote iliyopo imefunuliwa, kasoro hii haikufunuliwa. Lakini nikiwa nimekaa chumbani mwangu, na nikasikia hili au sio kusikia hilo, niseme, lakini niliona ikifunuliwa kuwa hizi ngurumo saba. Sasa hapo ndipo tuwezapo kufikia. Na naamini kwamba kila mmoja wenu mtamtumikia Mungu, na kufanya kile ambacho ni sahihi, na kumpenda Yeye maisha yako yote na kumtumikia, na Mungu atayasimamia hayo yaliyobaki.

Sasa katika kumalizia hapa sasa, kwa neema ya Mungu siri zote za mihuri sita ambayo ilikuwa imetiwa muhuri, na tunaolewa na kujua hapa kwamba muhuri wa saba haupaswi kujulikana hadharani.

Sasa kuja kwake, na saa ya kuja kwake, wakati dunia ikiharibiwa--- unajua, alisema pale “Ni nini itakayokuwa Ishara ya kuja kwako na mwisho wa dunia? Katika Mathayo 24, pale walipomuuliza hilo swali. Alienda kulijibu. Alieleza kuhusu waisraeli jinsi watakavyokusanywa kama Taifa katika mstari<sup>31</sup> ya Mathayo 24:31. Lakini alianza tena kwa mifano. Unaona? Unaona tena hapo, jifunzeni mifano ya mtini. Hapo tawi lake likiisha chipua na kuchanua majani, kwa nini, unajua kuwa wakati wa mavuno uko karibu. Na hapo “muonapo hayo yakitokea, hapo mnajua wakati u karibu”.

Waone waisraeli wakikusanyika katika nchi ya kwao. Lakini angalia. Aliacha Ufunuo wa huu muhuri wa saba. Na hapo wakati muhuri wa saba, alipoufungua huo, aliuwacha huo tena. Unaona? Kwa hiyo tunaona kuwa ni siri kamilifu, kwa hiyo, saa haijafika kwa ajili ya hizi siri kujulikana. Kwa hiyo, tumefikia umbali huu yaliyobaki yatajulikana hasa wakati ulio karibu na kuonekana kwa Yesu duniani tena kwa ajili ya Bibi Arusi wake, au chochote kitakachofanyika wakati huo.

Jambo lingine nataka mjue kile kilichotendeka. Na kama unasikiliza kanda ya “Je mabwana huu ndio wakati?” Mkiangalia mtaona Malaika mmoja alikuwa anamaanisha mno kwangu. Wale wengineo wote--- walionekana wa kawaida; lakini huyo Malaika alimaanisha sana kwangu. Alikuwa upande wangu wa kushoto katika ule mshikano wa piramidi waliounda wenyewe zile siri za Mungu zinajulikana tuu kwao. Na sasa walikuwa ni wajumbe waliokuja kunitafsiria ile piramidi au ule ujumbe wa

siri ya hii mihuri saba ambayo iko ndani ya hiyo piramidi.

Sasa, yule Malaika alikuwa upande wangu wa kushoto, ambaye ndiye hasa wa mwisho au Malaika wa saba, kama tutawahesabu wao kutoka kushoto kuelekea kulia, kwa sababu alikuwa kushoto kwangu. Mimi nikimuangali Yeye kuelekea magharibi, Yeye akija kuelekea mashariki naye atakuwa upande wa kushoto kwa hiyo huyo atakuwa ni mjumbe wa Malaika wa mwisho: ulimaanisha sana. Unakumbuka jinsi nilivyosema kwamba kichwa chake kama kiko nyuma, na mbawa zake kimechongoka, na vile alivyoruka kunijia mimi. Sasa, huo ni mhuri wa saba. Bado ni kitu kinachomaanisha. Na tu ---Hatujui ni kitu gani bado, kwa sababu haijaruhusiwa kuvunjwa [14]

Angalia. Nataka kusema jambo moja la ziada. Kwa karibu sasa, Usilikose hili. Jinsi linavyostaajabisha kutoka kwa ujumbe wa Malaika wa saba (Mjumbe wa muhuri wa saba) (Ufunuo 10 ilikuwa ni muhuri wa saba) mpaka kwenye zile baragumu saba, katikati ya hizi nyakati mbili--- [15].

Sasa, unabii huo kama unabii mwingine, una maana zaidi ya mmoja. Unabii wakati mwingine unamaana ya kimwili, halafu maana ya kiroho. [16].

Kumbuka unabii wowote una maana zaidi ya moja [17]. Na historia inajirudia yenyewe, na maandiko yana maana zaidi ya moja na Ufunuo zaidi ya mmoja. [4].

Sasa, ni vizuri niachie hapa. Unaona? Najisikia kama ninazuiwa nisiendele kusema zaidi juu ya hilo. Unaona? Kwa hiyo kumbuka tu, muhuri wa saba, sababu haukufunuliwa sababu iliyoacha isifunuliwe, hakuna anayetakiwa kujua lolote juu ya huo. Nataka mjue kuwa kabla sijajua hata Neno juu ya huo, hilo ono lilikuja miaka mingi iliyopita. Unakambuka hilo? Na hili hapa kama vile yale mengine..... linaungana na Neno moja kwa moja lilipo. Na Mungu anajua moyo wangu, kamwe sijawaza hata mara moja juu ya kitu kama hicho na hili hapa. Wakati umekwenda kuliko oh, mimi, inaonyesha tu kwamba inatoka kwa Mungu. Kwa hilo kuingia katika ahadi za Mungu kutoka mwisho wa ujumbe.

Angalia, angalia sasa, ile muhuri ya wakati wa mwisho, zaidi ya yote... Amefunua mihuri yote sita, lakini haisemi chochote juu ya muhuri wa saba. Na muhuri wa mwisho, utakapo anza, utakuwa ni siri kabisa kutokana na Biblia isemavyo. Kabla ya kujua hilo.... Na kumbuka Ufunuo sura 10:1-7. Wakati wa mwisho wa ujumbe wa Malaika wa saba, siri zote za Mungu zitakuwa zimefunuliwa/ zimejulikana. Tuko wakati wa mwisho kufunguliwa kwa muhuri wa saba [14].

Nukuu za kiingereza.

- [1] Nguvu za Mungu za kubadilisha (65-0911) Aya 77
- [2] Chakula cha kiroho cha wakati (65-0718E) Aya 83
- [3] Ile mbegu haitarithi pamoja na kapi (65-0218) Aya 101
- [4] Leo maandiko haya yametia (65-0219) Uk 22/9
- [5] Kujaribu kumtendea Mungu kazi (65-0718M) Aya 147/178
- [6] Wapakwa mafuta wa siku za mwisho(65-0725M) Aya 130/261-262
- [7] Nini kinavutia kule mlimani (65-0725E) Aya 146-149)
- [8] Kristo akifunuliwa katika Neno lake (65-0822M) Aya 162
- [9] Kunyakuliwa (65-1204), Aya 74-76
- [10] Wakati wa kanisa la laodikiaCAB Uk 327
- [11] Lile pengo kitabu cha mihuri Uk. 72-74
- [12] Ule muhuri wa Nne uk 283
- [13] Ule muhuri wa tatu uk235
- [14] Ule muhuri wa saba uk 574-578/564
- [15] Karamu ya tarumbeta (64-0719M) Uk 39
- [16] Madumadu, parare, tunutu, nzige (53-0612) Uk E-37
- [17] Ishara ya kimaandiko ya wakati (64-0410) Aya E-28

---

*jiwe la kiroho la kujengea na 178 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. [www.biblebelievers.de](http://www.biblebelievers.de)*

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,  
Box 553 Korogwe - Tanga  
E-mail: [Chaelika@livel.com](mailto:Chaelika@livel.com)  
Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*